# majira

GAZETI HURU LA KILA SIKU

www.timesmajira.co.tz

ISSN 0856-5086 ■ NA. 9327 • VOL. 6/9428

Alhamisi 4 • MACHI • 2021

BEI: TSHS 1000/KSHS 60


**Wajumbe UAE kutembelea viwanda vya kuchakata nyama nchini** Uk. 6

**BRELA yapongezwa kwa kuwafikia wajasiriamali** Uk. 2

**Serikali yaitaka TPA kuimarisha mitambo mita za upimaji mafuta** Uk. 4

**Ulanga wahakikishiwa kupata huduma ya maji safi na salama** Uk. 2

# Rais Dkt. Mwinyi ateua mawaziri

- **Ni aliyewahi kuwa Waziri wa Fedha wa Tanzania, makada wawili wa Chama cha ACT Wazalendo, kuapishwa leo** Uk. 4

## Waziri aamuru kufutwa hati, wananchi 74 kupatiwa eneo

Na Munir Shemweta, Nyamagana

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi amerejesha neema kwa wakazi wa Kata ya Mhandu katika halmashauri ya manispaa ya Nyamagana mkoa wa Mwanza kwa kuamuru... Inaendelea Uk. 4

## Mwanajeshi matatani kwa tuhuma za mauaji

Na Grace Gurisha

ASKARI wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Detective Copro, Jacob Silvester (34), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa... Inaendelea Uk. 3



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akimuuliza jambo Mhandisi wa Idara ya Mafuta, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Yona Malago wakati alipokagua mfumo wa mitambo ya mita za mafuta Kigamboni jijini Dar es Salaam jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

## Mfanyabiashara kizimbani akidaiwa kutakatisha mil. 850/-

Na Grace Gurisha

MFANYABIASHARA Manase Nakomolwa, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa... Inaendelea Uk. 3

# Maaskofu warejea wito wa tahadhari

Uk. 4

Scanned with CamScanner

# UAE kuja kutembelea viwanda vya nyama

**Na Mwandishi Maalumu**

BALOZI wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE) nchini, Khalifa Almarzooqi Abdulrahman amesema ataandaa wajumbe kutoka falme hizo kuja nchini kutembelea viwanda vya kuchakata nyama ili kujiridhisha na ubora wa nyama kwa ajili ya kupeleka katika nchi zao.

Akizungumza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, baada ya kumtembelea jana Dar es Salaam, balozi huyo amesema ni muhimu kwa viwanda vya kuchakata nyama vilivyopo nchini kupata soko la uhakika katika Nchi za Falme za Kiarabu kwa kuzingatia Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo Afrika.

Aidha, amewaasa wamiliki wa viwanda hivyo kuketi pamoja na kuwa na umoja wao katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ya kutafuta masoko ya bidhaa zao.

Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ndaki amemweleza balozi huyo kuwa viwanda vingi vya kuchakata nyama vinakabiliwa na changamoto ya masoko kupeleka bidhaa zao nchi za nje kutokana na kudaiwa kukosa sifa kulingana na baadhi ya sheria na kanuni zilizopo katika nchi hizo za kuingiza nyama kutoka nchi za nje.



"Viwanda vyetu vya kuchakata nyama licha ya kuwa na uwezo mkubwa wa kuchinja idadi kubwa ya ng'ombe, mbuzi na kondoo, lakini bado vinakabiliwa na changamoto ya kukosa masoko ya kupeleka bidhaa zao mara baada ya kuchakata nyama," alisema Ndaki

Kuhusu ujumbe kutoka UAE kuja nchini kutembelea viwanda vya kuchakata nyama na kujiridhisha na ubora wa bidhaa zinazozalishwa kama alivyoahidi balozi wao, alisema ujumbe huo utakuwa ni mwanzo mzuri wa viwanda hivyo kupata masoko ya bidhaa zao nchi za nje.

# umeme

# RAS apongeza wazazi kwa maziwa shuleni

**Na Oscar Job, Arusha**

KAIMU Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) wa Arusha, David Lyamunge, amewapongeza wazazi wa mkoa huo kwa kuitikia utaratibu wa utoaji wa lishe ya maziwa shuleni ulioanza kwa majaribio mkoani humo chini ya Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB).

Alisema kitendo cha wazazi hao chini ya kamati zao za shule kukubaliana kwa kauli moja kuanzishwa kwa mpango wa utoaji wa maziwa kwa ajili ya watoto shuleni, kinapaswa kuungwa mkono na wazazi wote.

Makubaliano hayo ya usambazaji wa maziwa shuleni baina ya bodi hiyo ya maziwa, wakuu wa shule 13 za mkoa huo, kamati za wazazi na TDB yamelenga kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maziwa shuleni.

"Mmekuwa mfano mzuri na kuigwa katika kufanikisha mpango huu ambao lengo lake ni kujenga afya za watoto shuleni pamoja kuboresha kiwango cha akili zao darasani.... Niwaombe wazazi na shule nyingine za mkoa huu kuiga mfano huu," alisema Lyamunge.

Alisema hatua ya kuanzishwa kwa mpango huo wa utoaji wa maziwa kwa utaratibu wa wazazi kuchangia kiasi kidogo cha fedha, pamoja na mambo mengine itasaidia kuongeza afya na uelewa wa wanafunzi shuleni na hivyo kufanya vizuri katika masomo.

Katibu tawala huyo wa mkoa aliwataka wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kuhamasisha shule ambazo hazijaanzisha mpango huo na kusisitiza kuwa, mkoa huo umedhamiria kufikia malengo ya kuhakikisha wanafunzi wote wa mkoa huo wanafikiwa na mpango huo.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa, Noel Byamungu, alisema mpango huo wa utoaji wa maziwa unaotekelezwa sasa katika Mkoa wa Arusha ukihusisha wanafunzi zaidi



ya 10,000 umelenga kuzifikia shule za msingi nchini kote.

Alisema chini ya mpango huo, TDB inasimama kama mratibu ambaye jukumu lake kubwa ni kuwaunganisha wazazi, shule pamoja na wenye viwanda ili kufanikisha mpango huo ambao kwa utaratibu, kila mzazi anachangia Sh 2,000 kwa mwezi kwa ajili ya ununuzi wa maziwa hayo yanayozalishwa viwandani.

Aliwaomba wazazi wenye watoto kuitikia kwa vitendo mpango huo ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na kusisitiza kuwa baada ya Mkoa wa Arusha, mpango huo unatarajiwa kwenda katika mikoa mingine wakianza na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Scanned with CamScanner

# Wajumbe UAE kutembelea viwanda vya kuchakata nyama nchini

**Na Edward Kondela**

■■BALOZI wa Falme za Nchi za Kiarabu (U.A.E) hapa nchini, Khalifa Almarzooqi Abdulrahman amesema ataandaa wajumbe kutoka U.A.E kuja hapa nchini kutembelea viwanda vya kuchakata nyama ili kujiridhishana ubora wa nyama kwa ajili ya kupeleka katika nchi zao.

Akizungumza jana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki, mara baada ya kumtembelea katika ofisi ndogo za wizara hiyo zilizopo jijini Dar es Salaam, balozi huyo alisema ni muhimu kwa viwanda vya kuchakata nyama vilivyopo hapa nchini kupata soko la uhakika katika nchi za Falme za Kiarabu kwa kuzingatia Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo.

Aidha, aliwaasa wamiliki wa viwanda hivyo kuketi pamoja na kuwa na umoja wao katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ya kutafuta masoko ya bidhaa zao.

Kwa upande wake Waziri Ndaki alimweleza balozi huyo kuwa viwanda vingi vya kuchakata nyama vinakabiliwa na changamoto ya masoko kupeleka bidhaa zao nchi za nje kutokana na kudaiwa kukosa sifa kulingana na baadhi ya sheria na kanuni zilizopo katika nchi hizo za kuingiza nyama kutoka nchi za nje.

"Viwanda vyetu vya kuchakata nyama lichaya kuwa na uwezo mkubwa wa kuchinja idadi kubwa ya ng'ombe, mbuzi na kondoo lakini bado vinakabiliwa na changamoto ya kukosa masoko ya kupeleka bidhaa zao mara baada ya kuchakata nyama."

Alisema Ndaki muhusu ujumbe kutoka Falme za Nchiza Kiarabu (U.A.E) kuja nchini kutembelea viwanda vya kuchakata nyama na kujiridhishana ubora wa bidhaa zinazozalishwa kama alivyoahidi balozi wa U.A.E hapa nchi.

Waziri Ndaki alisema ujumbe huo utakuwa ni mwanzo mzuri wa viwanda hivyo kupata masoko ya bidhaa zao nchi za nje.

Pia, Waziri Ndaki kuhusu sekta yauvuvi alimwambia balozi huyo kuwa Serikali iko katika hatua mbalimbali za kuhakikisha uvuvi wa bahari kuu unaanza katika ukanda wa Bahari ya Hindi kwa kujenga bandari ya uvuvi pamoja na ununuzi wa meli za uvuvi.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia) akiwa kwenye mazungumzo na Balozi wa Falme za Nchi Kiarabu (U.A.E) hapa nchini, Khalifa Almarzooqi Abdulrahman wakati balozi huyo alipofika katika ofisi ndogo za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zilizopo jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya mazungumzo na kumhakikishia kutuma ujumbe kutoka U.A.E kwa ajili ya kutembelea viwanda vya kuchakata nyama vilivyopo hapa nchini.** (Picha na Edward Kondela)

Scanned with CamScanner

# Waziri mifugo atoa angalizo uvuvi haramu

**NA REHEMA MAIGALA**

SERIKALI imesema haitomfumbia macho yeyote atakayefanya shughuli za uvuvi haramu kwa kuwa hauna tija katika nchi na ni hatari kwa ustawi wa sekta hiyo.

Akizungumza jana Dar es Salaam, wakati akifunga mkutano wa wadau wa sekta ya uvuvi Tanzania, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki, alisema uvuvi haramu haulipi na ukiendekezwa sekta hiyo haiwezi kukua kiuchumi.

Waziri Ndaki alisema uvuvi haramu una faida ya muda mfupi, lakini kukiwa na uvuvi halali utasaidia kukuza uchumi wa nchi siku zote.

"Tuvue samaki kwa uvuvi endelevu suala la uvuvi haramu tuachane nalo halina tija katika nchi yetu," alisema Ndaki.

Pia, aliwataka wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na bahari na maziwa wahakikishe wanatunza hifadhi za samaki.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Mifugo, Uvuvi na Kilimo Almasi Maige, alisema katika mikutano kama hiyo inatakiwa sheria zirekebishwe na kuongelewa kwa lugha ya kiswahili ili kila mtu aelewe kinachozungumzwa.

Alisema kuzungumzwa kwa lugha ya kiswahili kumesaidia kujua changamoto na faida nyingi za wavuvi katika mkutano huo.

Kwa upande wake Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda ambaye ni mdau wa sekta ya ufugaji, aliwataka wadau wenzake kuandaa ripoti ndogo ambayo ndani yake itakuwa imepewa mambo mazito ikiwamo kufufuliwa kwa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kuipeleka kwa Rais Dk. John Magufuli ili aone jitihada kubwa zinazofanywa katika sekta hiyo.

Scanned with CamScanner

**ASILIMIA 70>> Ni**

# Kibano kwa mabucha yasiyozingatia kanuni Bodi ya nyama yatoa mwongozo

**NA ASHURA ASSAD**

BODI ya Nyama nchini (TMB), imetoa mwongozo kwa mabucha ambayo hayafuati kanuni na utaratibu wa bodi hiyo, kutokana na ukaguzi wa mabucha katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Hatua hiyo imekuja baada ya bodi kubaini mabucha mengi hayazingatii matakwa ya sheria ya nyama katika uendeshaji wa biashara ya nyama.

Akizungumza na gazeti hili juzi jijini Dar es Salaam, Msajili wa Bodi hiyo, Imani Sichwale, alisema lengo la ukaguzi kwenye mabucha hayo lilikuwa ni kudhibiti ubora wa nyama nchini.

Pia, kudhibiti matumizi ya vifaa vinavyohatarisha usalama wa nyama, yakiwepo magogo, nondo za chuma zinazoshika kutu na usafi wa mazingira kwenye bucha, matumizi ya mizani ya mawe ambayo inasadikiwa kupunja wanunuzi wa nyama.

Aidha, alisema kutoa elimu na kuwasajili wadau mbalimbali wa tasnia ya nyama na kudhibiti uzalishaji wa nyama usiozingatia matakwa ya sheria za nchi.

“

**Kuna baadhi ya mabucha hayajasajiliwa na bodi na yanafanya biashara ya nyama bila ya kujua kanuni na utaratibu wa bodi juu ya sheria zake, hali inayosababisha kutokupatikana kwa ubora wa nyama kwenye mabucha...**

**Msajili wa Bodi hiyo, Imani Sichwale**

Kwa mujibu wa msajili huyo, wadau wengi wa nyama wanafanya biashara katika mazingira yanayokinzana na matakwa ya sheria ya nyama.

“Kuna baadhi ya mabucha hayajasajiliwa na bodi na yanafanya biashara ya nyama bila ya kujua kanuni na utaratibu wa bodi juu ya sheria zake, hali inayosababisha kutokupatikana kwa ubora wa nyama kwenye mabucha hayo,” alisema.

Alisema bodi ilibaini zaidi ya asilimia 70 ya mabucha yanatumia magogo ya miti kwa kuchakata nyama kinyume na maelezo ya serikali.

Msajili wa Bodi aliwasisitiza wafugaji kuhakikisha wanazingatia ufugaji wa kisasa ili mifugo yao iwe na ubora unaostahili.

Akizungumzia usalama wa nyama kwa mujibu wa sheria ya nyama, msajili huyo alisema wanaangalia nyama isiwe na wadudu waharibifu, isilete magonjwa na isiyoharibika kwa haraka.

Aliwasihi wafugaji kuhakikisha wanawatumia wataalamu wa nyama waliosomea ambao wanajua usalama wa mnyama kwa ajili ya matumizi ya binadamu, kabla ya kumchinja kwa lengo la kupata nyama bora.

Imani aliwataka wadau wa biashara ya nyama kuwa makini na utaratibu uliowekwa na bodi hiyo ili kuboresha sekta hii muhimu ya uzalishaji wa nyama.

# Deputy minister suspends head of cattle inspections

By Guardian Reporter

LIVESTOCK and Fisheries Deputy minister Pauline Gekul yesterday suspended the head of livestock inspections at Ruvu Darajani centre, Gabriel Lyakurwa for allegedly smuggling cattle, causing loss of government revenue.

She also directed the Coast Regional Commissioner Eng. Evarist Ndikilo to take to task staff of the Bagamoyo District Council who were colluding with the suspect.

Gekul made the decision after RC Ndikilo raised the allegations during the recent visit at the centre located in Bagamoyo District.

Ndikilo said his investigation revealed that the head of the centre had been collaborating with unscrupulous colleagues to smuggle livestock sent to the centre for inspection before being allowed to be taken to other auction stations.

"In my investigation I discovered that this smuggling involves a network of many people including some citizens, businessmen and civil servants. For example, on February 17, there were five vehicles that brought cattle to the centre for inspection, but only one vehicle went to Dar es Salaam as usual, while the rest of the herd was taken secretly to Kisarawe, Kibaha and Kidogozero village," the RC told the deputy minister.

Following the allegations, deputy minister Gekul suspended the official, saying that the ministry would set up a probe team to investigate the matter, including going through all the reports to determine how much government revenue was lost and all those found to be involved will be severely punished.

"We cannot embezzle government revenues, it is not possible to have more than 33 million head of cattle, but the contribution of the livestock sector to GDP does not exceed 7 per cent, it is because of games like this, we will not accept, and we will go to inspect all auction sites," she said.

Chalinze MP, Ridhiwani Kikwete urged the deputy minister to take serious measures to eliminate the entire network of criminals so that the council can earn big income.

Govt l...



## Tozo yawakimbiza wafanyabiashara wageni Soko la dagaa Kibirizi

## Prof. Ole Gabriel: LITA zalisheni wataalam watakaojiajiri

## ...ekul, amsimamisha kazi Mkuu wa kituo cha Ukaguzi wa Mifugo Ruvu darajani